



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA  
MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA



## TANGAZO KWA WAKUU WA VYUO VYA ELIMU YA JUU NA KATI

### KUSOGEZWA MBELE KWA TAREHE YA KUWASILISHA NAMBA ZA UTAIFA ZA WANAFUNZI WA VYUO VYA ELIMU YA JUU NA KATI KUWEZESHA UTAMBUZI WAO KWENYE VITUO VYA MATIBABU KWA ALAMA ZA VIDOLE

1. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) unapenda kuwajulisha Wakuu wa Vyuo vya Elimu ya Juu na Kati nchini kuwa umesogeza mbele tarehe ya mwisho ya kuwasilisha taarifa za Namba za Utaifa (NIDA) za wanafunzi wote wa vyuo vyao kutoka tarehe 15 Februari, 2023 iliyotangazwa awali mpaka tarehe **1 Aprili, 2023**.
2. Hili limefanyika kupisha nafasi kwa vyuo kukamilisha kipindi cha mitihani ya wanafunzi na kuwa na nafasi nzuri ya kulishughulikia hili.
3. Lengo la taarifa hizi ni kuwezesha uhakiki kwa alama za vidole (finger print) wa wanafunzi hao wakati wa kupata huduma za matibabu katika vituo vya kutolea huduma za afya vilivyosajiliwa na Mfuko ambao utanza tarehe **1 Aprili, 2023**
4. Kwa tangazo hili, Wakuu wa Vyuo vya Elimu ya Juu na Kati wanaombwa kuwasilisha taarifa hizo katika Ofisi za Mfuko zilizo karibu yao kabla ya tarehe hiyo ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza wakati wa kupata huduma.

Imetolewa na,

**KITENGO CHA UHUSIANO**

***Dodoma, Ijumaa, Machi 3, 2023***